


UTAFITI KUHUSU BINADAMU NA
MAZINGIRA AFRIKA YA MASHARIKI



NAMBA 1:

Uuzaji wa Maji Katika Jiji la Dar es Salaam

Marianne Kjellén



Imetolewa na Environment and Development Studies Unit
(EDSU), Chuo Kikuu cha Stockholm, Sweden

Stockholm University, Sweden, February 2000, ISSN: 1404-6784

Environment and Development Studies Unit (EDSU), School of Geography, Chuo Kikuu cha Stockholm, Sweden, inashirikiana na taasisi na mashirika ya utafiti mbalimbali Afrika ya Mashariki. Mpango wa Utafiti kuhusu Binadamu na Mazingira Afrika ya Mashariki una msingi wake kwenye utafiti unaofanyika na watafiti wa EDSU, pamoja na watafiti wa taasisi na mashirika yanayohusika Afrika ya Mashariki.

Makala hii ni makala ya kwanza katika orodha ya makala yanayohusiana na Mpango wa Utafiti kuhusu Binadamu na Mazingira Afrika ya Mashariki (ISSN 1404-6784). Utafiti kuhusu Uuzaji wa Maji Katika Jiji la Dar es Salaam, unatokana na mpango wa utafiti ujulikanao kwa jina la People, Provisioning and Place in African Cities (PPP) unaohusisha Department of Human Geography katika Chuo Kikuu cha Stockholm, na Department of Geography katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Zaidi ya Mpango huu wa Utafiti kuhusu Binadamu na Mazingira Afrika ya Mashariki, pia kuna Mpango wa Utafiti wa Binadamu na Mazingira Mikoa ya Kati Tanzania unaoendeshwa kwa ushirikiano kati ya EDSU na Institute of Resource Assessment (IRA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vyuho hivyo viwili vinashirikiana katika mipango mbalimbali ya kuandaa na kutekeleza shughuli za utafiti. Watafiti wapatao kumi na tano kutoka nyanja mbalimbali wanahusika na utafiti huu. Kwenye mpango wa Utafiti wa Binadamu na Mazingira Mikoa ya Kati Tanzania, wa EDSU na IRA, makala kumi na nne (ISSN 1104-5299) zimeshatolewa.

Mipango hii inagharamiwa na Department of Research Cooperation (SAREC) chini ya Swedish International Development Cooperation Agency (Sida). Orodha ya makala mengine yanayohusiana na mipango hii wa utafiti inapatikana Environment and Development Studies Unit (EDSU), School of Geography, Stockholm University, S-106 91 Stockholm, Sweden.

Tafsiri:

Maandishi ya makala hii yametafsiriwa katika Kiswahili na Emma Raymond.

Uuzaji wa Maji Katika Jiji la Dar Es Salaam

Makala ya Marianne Kjellén

Utangulizi

Tatizo la upatikanaji wa maji jijini Dar es Salaam ni jambo linaloeleweka. Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na matatizo makubwa ya maji. Baadhi ya kaya na wakati mwingine maeneo yote hayapati maji kutoka kwenye mabomba. Katika maeneo mengi pia msukumo wa maji ni mdogo. Malalamiko ya upungufu wa maji kwa Mamlaka ya Maji yamekuwa yakijitokeza hadi magazetini. Ni sehemu tu ya wakazi wa jiji la Dar es Salaam ambao hupata maji moja kwa moja kupitia kwenye mabomba. Wakazi wengi hupata maji kupitia watu wengine, ambao mabomba yao yanatoa maji au kutoka kwenye visima au kutoka kwenye sehemu maalum zinazotoa maji kwa jumuiya ambazo mara nyingi zipo mbali na nyumba.



Muza maji katika maeneo ya Tandale aktumia mkokoteni uliotengenezwa kwa chuma na matairi ya baisketi. Wauza maji wa aina hii, ni kawaida kuonekana kwenye maeneo mengi yenye makazi ya watu. Huwa wanachota maji kutoka kwenye nyumba zenye uhakika wa upatikanaji wa maji ya bomba. Bei ya maji ni shilingi 20 kwa chombo, nao wao huuza kwa shilingi 100 hadi 150 kutegemea na ugumu wa upatikanaji na usafirishaji maji. Kusukuma mkokoteni wenye vyombo vilivyojaa maji ni kazi ngumu, na wauza maji wengi walililamika kuwa wanapata maumivu ya viungo.



Hili ni mojawapo ya magari ambayo hutumika kusambaza maji kwa wakazi na wafanya biashara maeneo ya Oysterbay na Masaki. Magari haya hubeba kama lita 10,000 za maji. Kwa tanki lilojaa maji, bei ni shilingi 60,000 hadi 65,000. Watu wawili au watatu hufanya kazi kwenye gari hili ambalo linamilikwa na mtu binafsi.

Makala haya yanatoa matokeo ya utafiti uliofanywa kwa wauza maji wa jijini Dar es Salaam. Wauza maji hufanya kazi ya kupelekea watu maji majumbani mwao au kwenye sehemu za biashara amabazo hazina maji yanayotiririka kutoka kwenye mabomba. Sehemu kubwa ya makala hii imewalenga wauza maji kwa mikokoteni ingawa pia imetoa maelezo kuhusu uuzaji maji kwa kutumia magari yenye matanki. Utafiti huu ni sehemu ya utafiti mkubwa ambao unaangalia hali ya upatikanaji wa maji kwenye jiji lote la Dar es Salaam na pia kupitia mashirika mbali mbali. Kwa undani zaidi utafiti huu unalenga kwenye taratibu zinazohusika na matumizi na ugawaji wa maji.

Mfumo wa Maji wa Jiji la Dar es Salaam

Huduma ya kusafirisha maji kwa sehemu kubwa ya jiji la Dar es Salaam hutolewa na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka (DAWASA). Hata hivyo ni kama nusu tu ya wakazi wote wanapata huduma ya maji moja kwa moja kutoka kwenye Mamlaka ya Maji. Sehemu kubwa ya wakazi wa Dar es Salaam hupata huduma ya maji toka kwa watu binafsi. Zipo takwimu chache kuhusu hali halisi ya upatikanaji wa maji. Utafiti uliofanyika mwaka 1990 ulidai kwamba, kiasi cha asilimia 30 ya kaya

zote zilikuwa na mabomba ya maji yaliyounganisha hadi kwenye nyumba zao. Asilimia 25 ya kaya zilikuwa na mabomba yaliyounganishwa nje ya nyumba. Asilimia 45 ya kaya hazikuwa na mabomba, na kaya hizi zilitegemea zaidi mabomba ya wote au sehemu maalum za kuuzia maji. Hata hivyo siyo watu wote wenye mabomba wanapata maji kutoka kwenye mabomba yao kwa sababu katika maeneo mengi mfumo wa maji ya bomba haufanyi kazi. Baadhi ya watu pia wameunganisha mabomba ya maji kwa njia zisizo halali. Maeneo ya nje kidogo ya jiji hutegemea maji yanayotoka ardhini.


Kwa mtazamo wangu inaelekea kwamba kwa wakazi wengi wa Dar es Salaam hununua maji kutoka kwa majirani zao. Utafiti uliofanyika mwaka 1993 uligundua kwamba kati ya asilimia 80 na 90 ya kaya zote kwenye eneo hili la utafiti walikuwa wakinunua maji kutoka kwa majirani. Baadhi ya wakazi waliokuwa wameunganishiwa mabomba ya maji wamekuwa wakiwauzia maji wenzao. Katika maeneo ambayo hayana mabomba au upatikanaji wa maji si wa uhakika, wakazi wake wamekuwa wakichimba visima. Visima hivi vinatumika zaidi kwa ajili ya matumizi ya maji ya nyumbani na kwa kiasi kidogo maji hayo huuzwa kwa majirani. Wakati mwingine hata hivyo shughuli ya kuuza na kuhifadhi maji huwa ni kazi kubwa, na wasambazaji maji hununua maji ili kupeleka kwa wateja wao.



Wakazi wa nyumba hii wamejenga tanki kubwa sana la kuhifadhi maji na pia wanatumia mashine ya kusukumia maji ili kuhakikisha wanapata maji wakati wa mgao kwenye eneo hili.

Maji yanayohifadhiwa kwenye tanki huwa ni kwa ajili ya matumizi ya majirani siku ambazo hakuna mgao. Pia hufanya huwauzia maji wauza maji wa mitaani. Ukutani imeandikwa shilingi 20 kila ndoo.

Chimbuko la upatikanaji wa maji katika jiji la Dar es Salaam ni visima vya maji vilivyokuwepo jijini. Mfumo wa maji wa kwanza wa jiji uliandaliwa mwaka 1891. Kwa kutumia maji yaliyopatikana chini na juu ya ardhi, mfumo huo umekuwa ukipanuliwa kadri siku zilivyokwenda hadi kufikia katikati ya karne ya 1900. Uzalishaji wa maji kutoka Mto Ruvu, ambao ni tegemeo kubwa la sasa kwa jiji la Dar es Salaam ulianza miaka ya 1950. Mpango huu ulianza na mtambo wa maji wa Ruvu Juu, kama kilometa 65 Magharibi mwa Dar es Salaam. Huu mtambo wa maji kwa hivi sasa umeshafanyiwa upanuzi na ukarabati katika awamu mbalimbali. Mtambo wa maji wa Ruvu Chini ulianzishwa mwaka 1976. Maji mengi sasa yanapatikana kupitia mtambo huu. Lakini kati ya asilimia 10 hadi 20 ya maji yatolewayo na mtambo wa Ruvu Chini na theluthi mbili ya maji yatolewayo na mtambo wa Ruvu Juu yamekadiriwa kuwa yanapotea kwa sababu ya kuvuja kwa mabomba yanayosafirishia maji kabla hayajafika kwenye sehemu za kuhifadhia maji jijini. Kwa maana hiyo, ni maji mengi hutolewa na Mto Ruvu kuliko yale yanayofika mjini Dar es Salaam.




Kuna mtandao wa mabomba mkubwa wa kusafirishia maji ambao unahusisha sehemu kubwa ya jiji. Hata hivyo mfumo wa kati wa maji, kabla maji hayajapelekwa kwenye mabomba madogo madogo yanayoelekea kwenye nyumba za watu, bado haujaimarishwa vizuri.

Matokeo yake ni kwamba watu wengi huamua kuunganisha mabomba ya maji kwenye bomba kubwa. Hii inafanywa wakati mwingine kiholela bila ruhusa kutoka DAWASA na matokeo yake ni kusababisha kuvuja kwa maji.

Dar es Salaam ina mtandao mkubwa wa mabomba ya kusafirishia maji kwenda kwenye sehemu mbalimbali za jiji. Taarifa za wahisani zimeeleza kuwa hali ya mabomba ya kusafirishia maji kwa wastani ni ya kuridhisha. Lakini inabidi ieleweke kwamba, haya mabomba makubwa yanatakiwa yasaidiwe na mfumo wa mabomba ya maji ya wastani (kati) kwa ajili ya kusambaza maji kwa wakazi mbalimbali. Kutoka kwenye mfumo huu wa kati, uunganishwaji wa mabomba ya maji kupeleka

majumbani inabidi ufanywe kutumia mabomba madogo zaidi. Lakini hata hivyo, katika jiji la Dar es Salaam, huu mfumo wa kati wa maji bado haujaendelezwa ipasavyo. Kwa sababu hiyo, wakazi wa nyumba nyingi huunganisha mabomba ya maji kutoka kwenye mabomba makubwa ya kusafirishia maji. Kutokana na kukosekana kwa mfumo wa kati, kumekuwa na ongezeko la mtandao wa mabomba madogo madogo mengi ya watu binafsi ambayo husambaza maji kupelekea hadi nyumba zilizopo mbali. Mengi ya mabomba hayo madogo madogo ya kusambazia maji hayajatandazwa na kuunganishwa vizuri hivyo kusababisha kupasuka na kuvuja kwa mabomba hayo.



Mabomba madogo madogo ya kusambazia maji. Kama mfumo wa kati wa maji haujaimarishwa vizuri, watu wanalazimika kuunganisha mabomba kwenda majumbani kwao kutoka mbali na sehemu wanazoishi. Haya mabomba mara nyingi yanavuja na kusababisha madimbwi ya maji na kuruhusu maji machafu kuingia kwenye mfumo wa maji ya bomba.

Tatizo la kuvuja kwa maji kwenye mabomba ya kusambazia husababisha msukumo wa maji kuwa mdogo. Hivyo pamoja na kwamba watu wameunganisha mabomba kuelekea kwenye nyumba zao bado upatikanaji wa maji umekuwa ni wa matatizo. Baadhi ya wakazi wameunganisha mashine za kusukumia maji ili kuweza kupata maji majumbani mwao. Kwa jinsi ambavyo wameunganisha mabomba yao, yaani, kwa kupitia mabomba madogo madogo ambayo yapo ardhini,

inakuwa siyo tatizo kuunganisha mashine ya kusukumia maji. Katika maeneo ambayo wakazi hawana uwezo wa kugharamia mashine hizo za kusukumia maji, baadhi yao wamekuwa wakichimba mashimo ardhini ili kuunganishwa na mfumo wa usambazaji maji wa kwa mabomba ya chini ya ardhini.



Ili kuhakikisha kuwa wanapata maji, watu wengi wameunganisha mashine ya kusukumia maji kwenye mabomba yao. Hii inasaidia kuhakikisha kuwa mtu mwenye mashine anapata maji. Lakini hata hivyo, hii pia inasababisha kupungua kwa nguvu ya msukumo wa maji kwenye mfumo wa kusambaza maji. Katika maeneo wanayolishi wakazi wenye uwezo, mara nyingi ni watumishi wa nyumbani wanaotumika kushughulikia mashine za kusukumia maji.



Baadhi ya watu wanaoathirika kutokana na kupungua kwa nguvu ya msukumo wa maji, wamechimba na kutengeneza ngazi chini ya mabomba madogo ya kusambazia maji ambayo yametandazwa ardhini. Wakati msukumo wa maji kwenye hayo mabomba siyo wa kutosha kusukuma maji kupeleka kwenye mabomba yaliyotokeza juu, maji hutiririka kuelekea mabomba ya chini. Hili bomba la chini katika eneo la Tandika limejengewa vizuri na ngazi kwa kutumia saruji.

Ingawa sera ya maji Tanzania inayohusu upatikanaji bure wa maji haikutolewa kwenye sehemu za mijini, kodi za maji zimeshuka tangu kati kati ya miaka ya 1970. Makadirio ya matumizi ya maji yasiyo sahihi yamesababisha kodi ziwe chini ya kiwango kinachotakiwa. Tatizo hilo

pamoja na matatizo mengine yamesababisha kuifanya Mamlaka ya maji isiweze kutoa huduma ya maji inayotesheleza mahitaji ya wakazi wa jiji la Dar es Salaam.



Muuzaji maji anayefanya kazi Buguruni. Wauzaji maji kwa mikokoteni kwa kawaida ni vijana wa kiume ambao wana ujuzi wa awali wa shughuli za biashara ndogo ndogo. Wengi wao wamemaliza shule za msingi na wana mategemeo ya kupata ajira ya kudumu katika siku za usoni.

Uuzaji Wa Maji Dar Es Salaam

Unapoangalia takwimu za serikali na taarifa mbali mbali kuhusu huduma ya maji Dar es Salaam, unabaki kujiuliza “Wako wapi wauzaji maji ambao wanaonekana bayana kwenye mitaa ya jiji hasa katika pande za magharibi na kusini ya Dar es Salaam?” Takwimu nyingi haziantiki kwa undani kuhusu njia ambazo wakazi wa jiji wanatumia ili kupata maji. Pia mfumo mzima wa maji unapoelezewa kwenye taarifa mbalimbali, uuzaji wa maji unaofanywa na watu binasi huwa hauguswi. Kwa maana hiyo uuzaji wa maji unaofanywa na watu binafsi unasahauliwa kwenye mipango ya maendeleo ya jiji. Jambo ambalo inabidi lieleweke ni kwamba, uuzaji maji unasaidia kwa kiasi kikubwa vijana wengi kuweza kumudu maisha ya mjini. Pia shughuli hii ya kuuza maji, inatoa huduma ya maji kwa kaya nyingi jijini Dar es Salaam.

Utafiti huu una lengo la kuandika taarifa kuhusu shughuli nzima ya uuzaji maji ambayo imesahauliwa na wale ambao hawahusiki au hawajawahi kupata tatizo la maji. Ingawa utafiti huu ni mdogo kuweza kutoa habari kamili kuhusu ukubwa wa biashara hii ya maji, lengo ni

kuelewa ni jinsi gani shughuli za uuzaji maji zinavyofanywa na watu binafsi. Utafiti huu umetokana na kutembelea maeneo mbalimbali yanayohusika na uuzaji maji na kuhojiana na wauza maji 50. Mahojiano mengine yalifanyika kwa kwa wauza maji wakiwa kwenye kikundi. Sehemu ya kwanza ya utafiti ilifanyika miezi ya Septemba/Oktoba, 1998. Sehemu ya pili ya utafiti ilifanyika miezi ya Julai/Agosti, 1999. Mahojiano ya mwaka 1998 yalifanyika katika wadi za Temeke, Miburani (Tandika), Kipawa (Kiwalani) na Buguruni (Kwa Madenge) ambako pia mahojiano na kundi la wauzaji maji yalifanyika. Katika mwaka 1999, utafiti kwa njia ya mahojiano ulifanyika Ubungo (Kisiwani na Kibangu), Mabibo, Manzese (Muungano), Tandale, Kipawa (Kiwalani), Yombo (Vituka) na Kinondoni (mahali ambako magari ya matanki ya maji yanapatikana). Maeneo hayo yalichaguliwa kwa utafiti kwa sababu yalionekana kuwa na idadi kubwa ya wauza maji. Mahojiano yalichukua muda wa kama saa moja kwa kila mtu aliyohojiwa. Mahojiano hayo yalifanywa na mwandishi wa makala hii pamoja na watafiti wasaidizi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.



Katika maeneo ya Buguruni, baadhi ya wauza maji walihusika katika majadillano katika kikundi. Hapa wanaonyesha mauzo ya maji yanavyobadilika kufuatia misimu mbali mbali katika mwaka. Wakati wa kiangazi ambapo DAWASA inapata matatizo ya kusambaza maji ya kutosha kupitia kwenye mabomba kunakuwa na ongezeko la kazi kwa wauza maji. Ingawa kazi ni ngumu lakini wana furaha kwa kupata fursa ya kutengeneza pesa zaidi.

Kati ya waliohojiwa wote, 46 walikuwa wakifanya shughuli ya kusambaza maji kwa kutumia mikokoteni, wawili walikuwa wanatumia magari yenye matanki ya maji na wawili walikuwa wakiuza maji kwa wenzao kutoka majumbani mwao.

Usambazaji wa Maji kwa Mikokoteni

Wauza maji ni akina nani?

Wauza maji kwa kutumia mikokoteni kwa kawaida ni vijana wa kiume baadhi yao wakiwa bado wanasoma. Muuzaji maji mdogo kabisa kwa umri, alikuwa na miaka 15 na muuzaji maji mwenye umri mkubwa alikuwa na miaka 65. Umri wa wastani kwa wauzaji maji wote ilikuwa ni miaka 27. Wengi wa wauza maji walikuwa wamepata elimu ya shule ya msingi na baadhi yao walikuwa na elimu ya sekondari. Ni wauzaji watatu tu walikuwa hawajahudhuria shule ya msingi. Walipoulizwa kuhusu matarajio yao na kwa nini wameamua kuwa wauza maji, jibu lilikuwa ni ukosefu wa ajira “kazi hamna”. Hii inaonyesha kwamba, hamna aliyechagua kazi hii kwa ajili ya kupenda, isipokuwa ilikuwa ni shughuli ambayo ilionekana kuleta faida kuliko shughuli nyingine za biashara ndogondogo. Wengi wa wauza maji walikuwa na matumaini kuwa wangeweza kubadili kazi na kufanya shughuli nyingine za biashara au hata kupata ajira kwa siku za usoni.

Wauza maji walikuwa ni mchanganyiko wa watu wa makabila mbalimbali ya Tanzania. Kati ya wauza maji 46 wa mikokoteni, makabila 26 yalipatikana. Wauza maji wengi walikuwa ni wa kabila la kizaramo (wauza maji 6 kati ya wote waliohojiwa). Asilimia 65 ya wauza maji walikuwa bado hawajaoa. Kati ya hao ambao walikuwa hawajaoa ni mmoja tu ndiye alikuwa na watoto. Kati ya asilimia 26 ya waliokua wameoa, wengi wao walikuwa na mtoto mmoja mmoja tu, hata hivyo kwa baadhi yao idadi ya watoto ilikuwa ni kati ya 0 na 7.

Kama ilivyoielezwa awali, wauzaji wa maji kwa mikokoteni kwa kawaida ni wanume. Hata hivyo wanawake wawili wauza maji walipatikana wakati wa utafiti na wakahojiwa. Wakati hali zao kwa ujumla zilikuwa kama za wauza maji wa kiume, wao walionekana kuwa na upekee fulani kwa kuweza kujihusisha na shughuli zilizofanywa na wakazi wa jinsia tofauti. Wauza maji wengi wa kiume hawakuwa na habari ya kuwepo kwa wauza maji wa kike. Hata muuza maji mmoja wa kiume alisema kwamba “kama ukiona mwanamke anasukuma mikokoteni wa maji basi ujue maji hayo ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani”. Kwa kawaida wanawake huwa wanabeba maji kichwani.



Hawa wanawake wawili wauza maji ni wa aina yake kwa sababu wamevuka mipaka ya jinsia. Wakati ni kawaida kuona wanawake wamebeba maji, si jambo la kawaida wao kufanya hivyo kama shughuli ya biashara. Katika eneo moja kulikuwa na wanawake wengine ambao walijiunga, lakini inaelekea kwamba ni hawa wawili tu walokuwa na nguvu ya kuendelea na biashara hii ya maji.



Mama Khadija na Fatuma huza maji kwa wakazi wa maeneo ya Kilima Hewa. Hapa mtafiti yupo pamoja nao na mikokoteni yao.




Baadhi ya wauza maji wana vituo vyao vya mauzo nje ya maduka au kwenye maeneo ya mauzo ya mboga za majani. Kwa njia hii muuza duka na muuza maji wanasaidiana katika kuhudumia wateja wa kila mmoja wao. Picha hii imechukuliwa wakati wa utafiti Ubungo Kisiwani.

Kuna wakati wanawake wanabeba maji kwa mikokoteni (ingawa siyo jambo la kawaida), hata hivyo haikutarajiwa kwamba wangeweza kuuza maji hayo. Hata hivyo wauza maji wa kike wanaheshimika na wenzao wa kiume. Kwa wale waliokuwa wanawafahamu wauza maji hao wa kike walitoa maelezo mazuri tu juu yao.

Wauza maji wengi walionyesha kuwa uuzaji maji ndiyo shughuli pekee inayowapatia pesa. Hata hivyo, kama mmoja kati ya watano ya wauza maji walieleza kuwa wanajihusisha na shughuli nyingine zaidi ya kuuza maji. Baadhi yao walikuwa wakijihusisha na biashara ndogondogo kama kuuza mboga za majani na shughuli za ujenzi. Itakuwa si jambo la kutegemewa kuwa hawa wauza maji wanaweza kukataa kubeba mizigo ya aina nyingine wakiombwa. Lakini inavyoelekea ni kwamba, kwa sababu wengi wao wanatumia mikokoteni midogo yenye matairi ya baiskeli, wengi wao hawawezi kubeba mizigo mikubwa zaidi.

Mikokoteni au kwa majina mengine toroli au baiskeli ni vifaa muhimu vya kutendea kazi kwa wauza maji. Wengi wao wanamiliki mikokoteni, ila baadhi yao hukodisha magari na huwa wanalipa shilingi 500 kwa siku. Baadhi ya wauza maji waliona kuwa wanasaidiwa na wanaomiliki mikokoteni, lakini wengine wao waliona kuwa ni taabu



Muuzaji maji akionyesha mkokoteni wake ambao ni mkubwa kuliko kawaida, mbele ya nyumba yake, Ubungo Kisiwani.

kulipia mkokoteni wa kukodi kila siku. Wale wanaokodi mkokoteni pamoja na madumu ya kubebea maji hulipa hadi shilingi 1000 kwa siku. Karibu theluthi ya wauzaji maji walikuwa wameanza kwa kukodi vifaa vya kubebea maji. Lakini jinsi siku zilivyokwenda baadhi yao waliweza kujinunulia mikokoteni yao. Katika mazingira mengine imekuwa ni kinyume kwa baadhi yao. Wengine walianza shughuli hii wakiwa na mikokoteni yao, lakini baada ya muda mikokoteni iliibiwa kwa hiyo sasa inabidi wao ndio wakodi.

Upatikanaji wa Maji

Wauzaji maji kwa mikokoteni hufanya kazi yao zaidi kwenye maeneo ya magharibi na kusini mwa jiji la Dar es Salaam. Baadhi ya maeneo hayo yana mtandao wa mabomba lakini maji mara nyingi yamekuwa yakitolewa kwa mgao, katika siku au wiki. Kwa sababu hiyo wakazi katika kaya mbalimbali inabidi wanunue maji katika nyakati ambazo maji hayapatikani kupitia mabomba yao. Katika siku nyingine za wiki hupata maji katika mabomba yao. Pia baadhi ya maeneo watu wana mabomba lakini siyo wote wameunganishiwa mabomba kwenye mfumo wa maji. Wakazi katika maeneo hayo inabidi wanunue maji kutoka kwa majirani au wauzaji maji au labda kama wako tayari kutembea kufuata maji kwenye



Wakati wa matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji mwaka 1997, Wizara ya Maji pamoja na Mamlaka ya Maji walichimba visima virefu vya maji. Picha hii ilichukuliwa katika shule moja eneo la Temeke ambapo DAWASA wana kituo cha kuchotea maji. Mtumishi wa serikali hukusanya malipo.

mabomba ya wazi. Katika maeneo mengine hakuna kabisa mabomba, kwa hiyo wakazi inabidi wakachote kwa wale wenye visima au wanunue kutoka kwa wauza maji.

Wakati mwingine wauza maji hupata maji kutoka maeneo hayo hayo wanayouzia. Theluthi mbili ya wauza maji walitegemea kupata maji kutoka maeneo ambayo yanakumbwa na mgao wa maji. Kwa maana hiyo wauza maji, kama vile wakazi wengine katika maeneo hayo wanavyofanya ilibidi wakatafute maji sehemu nyingine. Maji hukatika kwa sababu ya mgao au kukatika kwa umeme. Tatizo la kukatika kwa umeme huathiri zaidi maeneo ambayo maji ya ardhini husukumwa kwa mashine za umeme.

Wauza maji mara nyingi hununua maji kwenye nyumba zinazouza maji au kutoka sehemu za mauzo ya maji kwa wote kupitia Mamlaka ya Maji. Wote hao hulipa pesa ili kupata maji. Uamuzi wa eneo la kuchotea maji unategemea zaidi umbali (Asilimia 52 ya wauza maji walitamka kwamba wanategemea zaidi maji yanayopatikana karibu nao). Ubora na uhakika wa upatikanaji wa maji pia ni sababu zinazochangia katika kuchagua sehemu ya kuchotea maji. Ni wawili tu, waliotamka kuwa bei ya maji kuwa ni kigezo cha uamuzi. Wengi wa wauza maji hutegemea maji yanayopatikana kwenye mabomba. Wale ambao walitegemea zaidi

kupata maji kutoka kwenye visima, hufanya kazi katika maeneo ambayo yapo mbali na mfumo wa maji wa jiji. Mara nyingi zaidi, wauza maji husambaza maji yanayopatikana katika mabomba ya wazi kwa wote. Katika maeneo yaliyopo nje ya mfumo huo wa maji, wauza maji wamekuwa wakitegemea wananchi binafsi ambao wamejichimbia visima virefu katika maeneo yao kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa maji. Katika maeneo hayo baadhi yao huweka hata dawa ya kuuwa vijidudu (Chlorine).

Wengi wa wauza maji walisema kuwa hakuna tatizo kubwa la upatikanaji wa maji. Wale ambao walisema kuwa upatikanaji wa maji ni wa taabu, tatizo kubwa lililojitokeza ni "kupanga foleni". Sababu nyingine zilizotajwa ni "kulowa maji", "vurugu" na uhotaji maji wa shida kutokana na ukosefu wa mpira wa kujazia maji. Kupanga foleni ni tatizo la mara kwa mara nyakati za asubuhi. Baadhi ya wauzaji walisistiza kwamba inabidi ufike sehemu ya kuchotea maji asubuhi na mapema. Kazi ya kupanga foleni ni tatizo lililojitokeza zaidi miaka ya nyuma. Katika maeneo yaliyopo nje kidogo ya jiji hali ya upatikanaji wa maji imekuwa



Katika maeneo yasiyokuwa na mabomba ya maji, baadhi ya kaya zimechimba visima na kuweka mashine za kusukumia maji za umeme. Wakati wa shughuli ya kufyatua matofali mmiliki wa nyumba hii aligundua kwamba wakazi wa maeneo yanayomzunguka wanahitaji maji. Hivyo alitengeneza visima vingi zaidi pamoja na tanki la kuhifadhi maji. Huweka dawa kwenye maji hayo. ya nafuu kidogo katika miaka ya karibu, au hasa ukilinganisha na miaka ya 1996 na 1997, ambayo inadaiwa ilikuwa ni miaka ya ukame. Unafuu

huo wa upatikanaji wa maji unatokana na kwamba idadi kubwa ya watu wamejichimbia visima vya binafsi na hivyo kuweza kuuza maji kwa majirani na wauzaji maji wa mitaani. Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), wahisani na DAWASA wamekuwa wakihusika pia na uchimbaji wa visima virefu. Ni maendeleo kidogo tu yalionekana katika upanuzi wa mtandao mzima wa maji kwa kutumia mabomba.



Katika nyumba hii, mwenye nyumba ametengeneza tanki la wazi ambalo hutumia kuhifadha maji na kuweza kutoa maji siku ambazo hakuna mgao. Mipira ya kumwagilia maji huwa inatumika kupitisha maji kutoka kwenye tanki na kujazia kwenye madumu.



Kuna shughuli kubwa ya ujenzi wa matanki ya maji inayoendelea ili kuimarisha upatikanaji wa maji. Tanki hili ambalo litatumika kuhifadhi maji linajengwa eneo la Yombo Kilakala kwa msaada wa "Water-Aid".

Usambazaji wa Maji

Kazi ngumu aliyonayo muuza maji ni kazi ya kusafirisha madumu yaliyojaa maji na kupeleka kwa wateja. Ilielezwa kwamba, tatizo kubwa ambalo wauza maji wengi walikumbana nalo wakati wakianza shughuli hii ni ugumu wa kazi yenyewe. Wengi wao walilalamika kuwa walipata maumivu ya kifua na viungo mbalimbali na mara kwa mara walipata homa. Kwa sababu wengi wao walianza kwa kukodi mikokoteni, hawakuweza kuanza shughuli hii taratibu, hivyo ilibidi wafanye kazi nzito kutwa nzima na baada ya hapo waliishia kulala tu. Muuza maji mmoja alieleza kwamba ilibidi kwa makusudi awe anapumzika siku moja kila baada ya kazi ya kutwa nzima ili "asichakae". Shughuli ya kusafirisha maji ni nzito pia kwa vifaa vinavyotumika kusafirishia maji. Hivyo tatizo kubwa la pili linalowakabili wauza maji ni kuharibika kwa mikokoteni. Tatizo hili linatokana na kupasuka kwa matairi na kupinda kwa rimu. Barabara zikitengenezwa vizuri kwa mfano kuwekwa lami

zinaweza zikarahisisha usafirishaji kwa kiasi kikubwa, kwa sababu kazi ya kuvuta mkokoteni kwenye mchanga ni ngumu sana. Hata hivyo barabara zinapokuwa nzuri, kuna hatari ya kuongezeka kwa ajali za barabarani, hivyo mikokoteni pia inakuwa kati hali ya hatari.



Huu ni mkokoteni mkubwa sana wenye matairi ya gari. Una uwezo wa kubeba madumu ishirini. Huu mkokoteni ukijaa ni mzito sana na unatumika zaidi kwa ajili ya kukusanyia maji kuliko kusambazia.

Mikokoteni mingi huwa ilionekana kuwa na uwezo wa kubeba madumu ya maji 6 (asilimia 44), 7 (asilimia 21) au 8 (asilimia 14). Asilimia 90 ya wauza maji walikuwa na mikokoteni yenye matairi ya baiskeli. Wachache walikuwa na mikokoteni ya pikipiki (asilimia 7) na matairi ya gari (asilimia 4). Mikokoteni ya namna hii ina uwezo wa kubeba kama vyombo vya maji (madumu) 20 hadi 30. Kila chombo kina uwezo wa kubeba lita 20 hadi 25 za maji. Mzigo wa madumu 7 yenye lita 25 za maji una uzito wa kilo 175, "ongeza uzito wa chuma au mkokoteni wenyewe!" Kwa maana hiyo, wauzaji wengi wa maji, hupendelea kuuza maji kutoka kwenye kituo maalumu na kupeleka kwa mteja pale wanapoitwa. Kuliko kuzunguka na mzigo mzito wa maji.

Kutokana na maelezo ya wauza maji, wateja wanaonekana kuridhishwa na huduma hiyo ya maji. Ni asilimia 9 tu ya wauza maji walisema kuwa huwa wanapata malalamiko toka kwa wateja mara kwa mara. Asilimia 49 walisema malalamiko huwa yanatokea mara chache, na asilimia 42 walisema kuwa kulikuwa hakuna malalamiko yoyote yale kutoka kwa wateja. Tena wengine walisisitiza kuwa wateja huwa wanashukuru sana kwa huduma hii ya maji. Hata hivyo, ilielezwa kwamba malalamiko yanayojitokeza mara kwa mara huwa yanasababishwa na ucheleweshaji wa maji. Kwa kawaida, wauza maji wakishapewa agizo la kuleta maji, hukubali na kukimbia mara moja. Lakini hata hivyo wakati mwingine wauza maji hao hukumbana na matatizo yasiyotabirika ya foleni ndefu au ugumu wa kuyapata hayo maji. Katika mazingira kama haya wauza maji wengine huwasaidia wenzao.

Wauza maji kadhaa walieleza kuwa kama mwenzao amepata agizo la kuleta maji, wenzake waliweza kumsaidia apite mbele, yaani asisimame foleni. Na pia ilielezwa kwamba kama mkokoteni wa mmoja wao ulikuwa umeharibika, wenzake walimsaidia kupeleka maji. Lakini kwa wakati mwingine pia huwa kunakuwa na mashindano, na kuna uwezekano wa wauza maji wengine kumuongelea vibaya mwenzao kwamba maji anayosambaza siyo safi.


Ilielezwa pia wateja wengine hulalamika kama wameletewa kiasi kidogo cha maji kuliko walivyotegemea. Kwa sababu hii, wauza maji wengine walikuwa na vyombo vidogo vya maji ambavyo vilitumika kujazia maji kwenye madumu ili kuhakikisha kuwa mteja anapata dumu lililojaa maji. Malalamiko mengine kutoka kwa wateja yalikusiana na usafi wa maji, rangi au chumvichumvi au kutokuwa na imani ya usalama wa maji kutokana na sehemu yanapochotwa. Wauza maji kwa kawaida hutumia madumu ya meupe (ambayo ni makubwa na ni ya gharama) au madumu ya njano (ambayo awali yalitumika kuwekea mafuta ya kupikia). Ilielezwa kwamba, wateja wanapendelea zaidi madumu meupe, kwa sababu yana uwezo wa kuonyesha uchafu kwa urahisi.



Picha hii iliyochukuliwa Tandale inaonyesha toroli dogo sana. Chombo kidogo kwenye mshikio wa toroli hutumika kujazia maji kwenye madumu mengine ili mteja aweze kupata ujazo kamili wa maji kulingana na pesa aliyolipa.

Usambazaji wa Maji kwa Magari

Wakati usambazaji maji kwa mikokoteni ni aina ya ajira binafsi kwa ajili ya kutoa huduma ya maji kwa wakazi wenye kipato cha chini, usambazaji kwa kutumia magari yenye matanki ya maji una utaratibu maalum na unahudumia zaidi maeneo yenye watu wenye kipato cha juu. Wateja wao kwa ujumla ni kaya zenye uwezo, wataalamu kutoka nje na sehemu za biashara ikiwa ni pamoja na mahoteli makubwa. Upelekaji wa maji huo



Waendesha magari ya maji mara nyingi huhudumia sehemu za watu wenye uwezo. Baadhi ya wateja husimamisha magari yao na kuwaelekeza wenye magari ya maji majumbani kwao. Wengine, kama inavyoonyeshwa kwenye picha wanaagiza kwa njia ya simu. Wateja wengi huwa wanaagiza mapema ili wapate huduma hiyo mara moja au mara mbili kwa wiki.

na malipo yake hufanywa kwa kutumia taarifa za madai. Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) huwa inatozwa kwenye mauzo. Pia wateja huwaendea wenye magari hayo kwa ajili ya kupata maji mara moja moja. Bei huwa ni mapatano.

Mengi ya magari ya kusambaza maji huwa yanajipanga katika kituo cha kujazia maji cha DAWASA kilichopo karibu na kanisa la St. Peters, katika Wilaya ya Kinondoni. Sehemu yao kubwa ya mauzo ya maji ni Masaki karibu na ufukoni mwa Bahari ya Hindi, eneo ambalo pia watu wenye kipato cha juu wanaishi. Ingawa upatikanaji wa maji unategemewa kuwa uwe wa uhakika kwa sababu siyo mbali na mtambo wa Maji wa Ruvu Chini (au kama unavyoitwa na wengi "Bomba la Ikulu"), bado maji yapatikanayo hayatoshelezi. Hii ni kwa sababu mabomba yaliyounganishwa ni ya plastiki na yanavuja sana na kusababisha msukumo mdogo wa maji. Hali hii inasababishwa zaidi na kuwepo kwa mashine za kusukumia maji ambazo zinatumiwa kwa wingi katika nyumba na mashirika mbalimbali.

Hali ya upungufu wa maji katika maeneo ya watu wanaojiweza hata hivyo ni jambo linaloshughulikiwa na Mamlaka ya Maji. Tanki la kuhifadhia maji limejengwa Msasani Peninsula na baadhi ya

matengenezo yapo mbioni kufanyika. Wahudumu wa magari ya kusambaza maji, walionyesha hofu yao kuwa, matengenezo yatakayofanyika yanaweza yakasababisha watolewe nje ya biashara, kwa sababu upatikanaji wa maji utakuwa siyo tatizo tena. Pia wengine walihisi kwamba ubinafsishaji wa Mamlaka ya Maji unaotarajiwa kufanyika utaathiri biashara yao. Inaonekana kwamba, Mamlaka ya Maji ikibinafsishwa, katika misingi ya biashara, kampuni mpya itakayokuja nayo itanza kuhudumia wakazi kwenye maeneo hayo hayo ya watu wenye uwezo.



Magari mengi ya kubebea maji huwa yanapatikana karibu na kantsa la St. Peters, Kinondoni. Waendesha magari huwa wanajaza maji kwenye matanki yao, na wanaohitaji maji wanajua jinsi ya kuwapata. Kwa sababu waendesha magari wana kituo maalum cha kujazia maji, hutumia pia fursa hiyo kuzoeana na wenzao. Wengi wao walionyesha kuwa wana ushirikiano mkubwa ingawa pia kwa wakati huo huo ni washindani wa biashara.

Yapo kama magari 20 ya kusambaza maji yanayofanya kazi jijini Dar es Salaam. Mengi ya magari hayo yanamilikiwa na watu binafsi. Makampuni makubwa ambayo huwapatia maji wafanyakazi wake pia yanahusika na uendeshaji wa haya magari. Ukubwa wa magari unatofautiana, lakini kwa wastani, magari mengi yana ujazo kati ya lita 9,000 na 10,000.

Bei za Maji

Bei za maji katika soko huria zina kawaida ya kuwa juu kuliko bei za serikali za kulipia maji kwenye Mamlaka ya Maji. Nyumba ambazo zinapata huduma ya maji moja kwa moja kutoka Mamlaka ya Maji hulipa bei ndogo. Mara nyingi bei hizo zinapangwa kwa mwezi bila kujali kiasi halisi cha maji kilichotumika. Hali hii inasaidia watu wanaouza maji kwa wenzao. Hata hivyo watu wengi niliozungumza nao wakati wa utafiti walieleza kuwa bili za maji zimekuwa zikiwajia pamoja na kwamba wamekuwa hawapati maji kupitia mabomba yao kwa miaka kadhaa.

Kodi za maji za serikali zinatofautiana kutegemea na aina ya watumiaji. Kodi hizi zinatumiwa katika kuandaa taarifa za madai ya maji kwa wenye mita (sehemu ambazo Mamlaka ya Maji inaelewa kiasi cha maji kilichotumika) na kupanga kiwango maalum cha madai (ambapo Mamlaka ya Maji hufanya makadirio ya maji yaliyotumika kutokana na maji yaliyosambazwa kwenye eneo lote). Katika mwaka 1997/1998 kodi hizo zilikuwa kama ifuatavyo: shilingi 0.20 kwa lita moja ya maji kwenye nyumba za watu binafsi, shilingi 0.30 kwa serikali, shilingi 0.40 kwa makampuni ya biashara na viwanda na shilingi 1.10 kwa wataalamu kutoka nje. Kiwango cha juu kabisa cha serikali kiliwekwa kwa magari ya matanki ya maji, ambapo malipo kwa Mamlaka ya Maji yalikuwa ni shilingi 3.80 kwa lita.

Gharama na Mapato ya Wasambazaji Maji kwa Magari

Ukiacha DAWASA, watoa huduma ya maji wengi huwa hawana bei maalum, bei huwa ni mapatano. Ilielezwa kwamba bei za maji zinategemea zaidi gharama za uendeshaji. Gharama hizo ni kama ifuatavyo:

- Maji: gharama yake ikiwa ni shilingi 3.80 kwa lita mwaka 1998 na shilingi 4.80 kwa lita mwezi Julai, 1999. Hivi karibuni ilionekana pia kuna nyumba ambazo huwauzia maji wenye haya magari kwa bei ya shilingi 10,000 kwa lita 10,000 za maji. Bei ya serikali ambayo ingetakiwa ilipwe kwa Mamlaka ya Maji kwa kiasi hicho cha maji ni shilingi 48,000.
- Mafuta: Hii inafanya bei ya mauzo itofautiane kutegemea umbali kutoka kituo cha kujazia maji. Lita 10,000 zinaweza zikauzwa kwa shilingi 60,000 hadi 65,000 karibu na Oyster bay, na shilingi 75,000 Makongo Juu, kama kilometa 10 kutoka kituo cha kujazia maji.
- Vibarua: Kwa kawaida dereva anayeendesha gari la kubeba maji huwa anakuwa na wasaidizi wawili.
- Gharama za matengenezo ya gari na kiwango cha faida alichojiwekea mwenye gari.

Kwa mteja anayenunua maji, bei inayolipwa kwa muuza maji inaweza ikawa kiasi cha shilingi 6.00 hadi 6.50 kwa lita moja kwa maeneo ya Oyster-bay na kama shilingi 7.50 kwa Makongo Juu. Wanaotegemea maji yanayosambazwa na magari mara nyingi ni wafanya biashara wakubwa au wakazi wengine wenye uwezo.

Gharama na Mapato ya Wauza Maji kwa Mikokoteni

Uuzaji wa maji kutoka katika kaya moja kwa kaya nyingine ni kitu cha kawaida sehemu ambapo si wote wameunganisha mabomba. Bei ya maji kwa wauzaji binafsi kwa njia hii huwa ni shilingi 20 kwa ndoo (kwa kama lita 20 za maji). Hii ni sawasawa na shilingi moja kwa lita moja. Hata hivyo bei zinatofautiana katika sehemu mbali mbali, na pia zinategemea uhusiano kati ya majirani. Gharama ya ununuzi wa maji kwa chombo chenye zaidi kidogo ya lita 20 ilikuwa ni kati ya shilingi 10 na 40. Asilimia 50 walilipa shilingi 20 kwa chombo, asilimia 30 walilipa chini ya hapo na asilimia 20 walilipa zaidi ya hapo. Matokeo yake ni kwamba gharama ya kununulia maji kwa wasambazaji maji kwa wastani ilikuwa chini ya shilingi moja kwa lita.

Bei ya rejareja kwa wauza maji wa mikokoteni majumbani na wateja wengine ilitofautiana katika sehemu mbalimbali za jiji. Bei ya maji kwa kawaida ilikuwa shilingi 100 kwa dumu lenye lita 20 na zaidi bei ambayo ni sawasawa na shilingi 5 kwa lita. Asilimia 67 ya wauza maji walitumia kiwango hiki kama bei yao ya kawaida ya mauzo. Maeneo ya Temeke (Ghorofani) ambapo maji yanatolewa kwa mgao unaokuja kwa saa, mara mbili kwa siku, bei ya maji ilikuwa ni ya chini zaidi kuliko sehemu zote. Bei hiyo ilikuwa ni shilingi 70 kwa chombo, na wateja wa kila siku walipata maji kwa shilingi 50 kwa chombo. Bei kubwa ya maji ilikuwa kwenye maeneo ambayo yalikuwa mbali na sehemu ambapo maji hupatikana. Katika maeneo ya Kiwalani, ambapo mabomba ya maji ni machache sana, mauzo ya maji yalikuwa shilingi 150 kwa chombo. Maeneo ya juu kama Ubungo Kibangu mauzo maji yalifikia hadi shilingi 200 kwa chombo. Maeneo kama Buguruni na Manzese, bei ya maji ilikuwa kama shilingi 100, kutokana na sababu kwamba maji yalipatikana karibu. Kwa sababu mgao wake ulichukua muda mrefu kabla maji hayajapatikana tena. Hali hii ilifanya wauza maji watembe umbali mrefu katika baadhi za siku. Familia zilizotegemea wauza maji kwa mikokoteni zililipa kati ya shilingi 2.50 na 10 kwa lita moja ya maji, kama gharama ya kupelekewa maji majumbani kwao.

Kiasi cha maji kinachouzwa ni vigumu kukisiwa. Kwanza kinatofautiana sana na inakuwa vigumu kwa wauza maji kukumbuka zaidi ya bei ya maji. Pia inawezekana kwamba wengi waliona kuwa ni kama dhahaka kwa Mungu kujaribu kukadiria mauzo yao ya baadaye.

Hata hivyo wauza maji wengi walieleza kuwa kwa wastani wanaweza kuchota maji kama mara tatu kwa siku. Kwa “siku nzuri”wastani huwa kama mara nne na “siku mbaya” mara moja au mbili. Hii ni kwa sababu wengi wao huwa hawana kazi kabisa siku ambazo mvua inanyesha au maji yanatoka bombani kwa sehemu zile zenye mgao wa maji.



Mvua ikinyesha wauza maji huwa na kazi kidogo kwa sababu wakazi kwenye nyumba nyingi hukinga maji ya mvua kwa ajili ya mahitaji yao. Wakazi wa nyumba hii Ubungo Kibangu wamejiandaa kuosha vyombo vyao na maji ya mvua wakati wowote maji yatakapopatikana.

Kwa kawaida wauza maji hujaza kama vyombo 18 vya maji (kama safari 3) kwa siku. Katika utafiti huu ilionekana kwamba kiasi cha maji yaliyouzwa kilikuwa kama kati ya vyombo 6 na 90 vya maji (kama kuna wasaidizi), na wastani wa vyombo 26. Hata hivyo ieleweke kwamba wauza maji hawaweki mahesabu katika vitabu. Mahojiano kuhusu mapato yalichukuliwa kwa hisia mbalimbali na inawezekana kuwa wengine walifanya ni siri kwa kuhofia ushuru. Hata hivyo muuza maji wa kawaida anaweza akawa na mapato ya shilingi 1,600 kwa siku baada ya kutoa gharama ya kununua maji. Kama mkokoteni ni wa kukodi, huo unaweza ukagharimu shilingi 500 kwa siku, hivyo matokeo yake ni mapato ya shilingi 1,100 kwa siku. Kwa kufanya kazi kwa siku sita kwa wiki mapato yanakuwa ni shilingi 6,600. Ukitoa gharama za matengenezo ya mkokoteni ya shilingi 600 (matengenezo ya mkokoteni hugharamiwa na muuza maji hata kama yeye siyo mmiliki wa mkokoteni), mapato

kamili ya wiki yanaweza kuwa shilingi 6,000. Ukizidisha mara nne, mapato ni shilingi 24,000, kipato hicho kipo chini kidogo ya kima cha chini cha serikali kwa mwezi ambacho ni shilingi 30,000.

Ingawa mapato hayo yaliyoonyeshwa hapo juu yametokana na mahesabu ya kiwango cha chini cha uuzaji na kiwango cha juu cha gharama (kama kukodi mkokoteni), hii bado inaonyesha wazi kwamba kazi ya kuuza maji siyo biashara ya kumpatia mtu kipato cha kutosha. Katika hali hiyo, ni nusu tu ya wauza maji waliosema kwamba shughuli hiyo inawawezesha kuwapatia mahitaji yao ya kila siku. Vilevile, asilimia 61 ya wauza maji walisema kwamba angalau waliweza kupata chakula cha kuwatosha. Asilimia 17 walisema hulala na njaa mara moja moja na asilimia 22 walidai kwamba mara nyingi hulala na njaa. Pamoja na kipato cha wastani, wengi wao (asilimia 66) walisema waliweza kuhifadhi pesa kama “akiba ya tahadhari”.

Hitimisho

Jitihada za watu binafsi kama vile uuzaji maji ni njia ambayo inasaidia kupambana na matatizo yanayotokana na mfumo mzima wa usambazaji maji kwa wananchi. Shughuli kama hii inatakiwa ionekane kama ni huduma ambayo inawazesha wakazi wa jiji kupata mahitaji yao ya maji. Wauza maji wanakuwepo kwa wingi katika maeneo ambayo hayana uhakika wa upatikanaji wa maji, hii ikiwa ni pamoja na sehemu za biashara na makazi ya watu wenye uwezo wa kulipa huduma ya maji. Katika maeneo ya watu wenye kipato cha chini sana, pamoja kuwa na tatizo la upatikanaji wa maji, uwezekano wa upatikanaji wa wauza maji unakuwa pia ni mdogo. Katika hali kama hiyo wanawake na watoto wanatumika sana ili kukabiliana na tatizo hilo. Hata hivyo wakazi hao wenye kipato cha chini inabidi walipie gharama kubwa kwa ajili ya maji, kwa vile ni vigumu kukuta sehemu ambapo maji yanapatikana bure.



Kama miaka kumi iliyopita, kulikuwa na mabomba mengi ya jumuiya yaliyotoa maji ya bure kwa wakazi wa jiji. Hata hivyo, kwa siku za hivi karibuni ni vigumu kuona mabomba kama hayo. Picha hii inaonyesha bomba la maji ambalo ilielezwa kuwa lilivunjwa kwa makusudi.

Katika mtazamo wa kiafya, njia yenye ufanisi zaidi katika kutoa huduma ya maji kwa wakazi wote ni kupitia mabomba ya maji. Ikiwa wakazi wa jiji itabidi wabebe maji yote yanayohitajika nyumbani, ni hakika kwamba usafi wa watu na mazingira utaathirika. Hata hivyo kuweza kuunganisha mfumo wa mabomba ya maji kwa kila kaya jijini Dar es Salaam ni jambo lisilowezekana kirahisi katika kipindi kifupi. Hivyo njia ambazo zinaweza kufaa kuboresha mfumo mzima wa maji kwa wakazi wa jiji inabidi zipatikane.

Uuzaji wa maji unaofanywa na watu binafsi jijini Dar es Salaam ni shughuli ambayo inakua na muhimu kwa wakazi wengi kutokana na mahitaji. Ili kuweza kusaidia kupunguza gharama za maji zinazotolewa na wauza maji, wahuusika na huduma ya maji inabidi watoe kipaumbele usambazaji wa maji kwa uhakika katika maeneo yaliyoathirika zaidi. Tofauti ya bei kiasi kikubwa inategemea umbali kutoka sehemu maji yanapopatikana. Katika maeneo yenye watu wenye kipato cha chini, bei kubwa za maji ni kikwazo kikubwa kwa kaya zenye hali duni. Ikiwa ugumu wa shughuli ya uuzaji maji inaweza ikapunguzwa, bei za maji kwa wateja zinaweza zikapungua.



Uuzaji wa maji, mbali na kusaidia kuongeza kipato cha watu, ni shughuli inayosaidia upatikanaji wa maji usio na matatizo makubwa. Ingawa si huduma ya kirahisi kwa wateja, shughuli hii inagharimu mtaji kidogo kuna uwezekano wa kubadilika kulingana na mahitaji ya wateja. Uuzaji maji unatakiwa uonekane kama ni mwendelezo wa mfumo wa usambazaji maji wa bomba.

Tatizo kubwa linalowakabili wauza maji, ukiacha umbali, ni hali mbaya za barabara (kutokana na mchanga). Barabara zikitengenezwa vizuri, kama kuwekwa lami, kazi ya usambazaji wa maji inaweza kuwa rahisi kidogo na gharama ikapungua, ingawaje hatari za ajali za barabarani zitakuwepo. Bei za maji kwa wateja zinakuwa chini katika maeneo yenye mgao wa maji ambapo maji hupatikana mara kwa mara kuliko maeneo ambayo inachukua kipindi kirefu kabla watu hawajapata maji. Kwa hiyo DAWASA, kwa njia ya kutoa mgao zaidi wanaweza kufanya bei za uuzaji maji kwa watu zipungue.

Uuzaji maji ni shughuli ambayo inatoa jawabu la muda mfupi, pia inatoa msaada kwa wote walio na uwezo wa kulipia. Kwa kusema kweli, huduma ya maji ya bomba siyo gharama sana ukilinganisha na kununua maji kutoka kwa watu binafsi isipokuwa tu ni kwamba inahitaji mtaji mkubwa. Uuzaji wa maji wa mitaani ingawa unahitaji mtaji mdogo kwa wauzaji lakini gharama zake ni kubwa kwa wateja ambao hubidi wanunue maji kila siku. Hata hivyo kama ilivyoelezwa hapo awali ni kwamba huduma ya maji ya bomba kwa watu wote siyo rahisi katika kipindi kifupi.



Wakati nguvu ya msukumo wa maji imepungua, kazi ya kukinga maji inachukua muda mwingi sana. Hawa wanawake wanachota maji kwenye kisima kirefu kilichopo Kipawa, ambacho kilichimbwa siku za nyuma kwa msaada wa Médecins sans Frontières. Bei ya maji ni shilingi kumi kwa kila chombo

Kwa kifupi, usambazaji wa maji kwa watu wote kwa kuweka mabomba mengi ya wazi kwa wote, kuimarisha mgao wa maji ili usipite muda mrefu bila maji, kukabiliana na tatizo la kuvuja mabomba ya maji (linalosababisha msukumo mdogo wa maji) ni njia muhimu za kukabiliana na mataizo yaliyopo kwa wakati huu. Bila shaka wakazi wengi wa jiji wataafikiana na hili, na kwa upande mwingine wauza maji pia. Mfumo kamili wa usambazaji maji kwa mabomba hatimaye unaweza ukawaondoa wauza maji kutoka kwenye biashara, hii ni hofu kubwa iliyojitokeza kwa baadhi ya wauza maji. Jambo la msingi hata hivyo ni kwamba, uuzaji maji ni mwendelezo wa huduma ya maji kupitia katika mfumo wa mabomba. Hivyo inabidi kuwepo na ushirikiano mzuri kati ya DAWASA na wauza maji binafsi.



Mwandishi wa makala haya akipumzika pembeni mwa reli ya TAZARA.

Shukrani

Ninapenda kuwashukuru watu wote walionisaidia katika utafiti huu. Kwanza, watu wote waliokubali kuhojiwa, pamoja na viongozi wote walionisaidia katika maeneo yao. Shukrani zangu pia ziende Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kunipatia msaada katika mahojiano kwa kushirikiana na Mathias Ngowi na Novatus Luanda. Fedha kwa ajili ya safari hii zimetolewa na Ahlmanns and Lagrelius Fund for Geographic Research (1998) na SAREC (1999). Bila ya wote hawa, utafiti huu usingeweza kufanyika. Kwa pamoja ninasema “Ahsante Sana”

Maelezo

Mradi wa utafiti huu unaitwa “Institutional Forms of Water Provisioning in Dar es Salaam, Tanzania”. Kama una maoni au ukitaka maelezo zaidi juu ya matokeo ya utafiti huu, tafadhali wasiliana na:

Marianne Kjellén,
Stockholm University,
Department of Human Geography,
S-106 91 Stockholm,
SWEDEN.